



## KUHUSU GNI

Global Network Initiative (GNI) ni jukwaa la washikadau wengi linalowaleta pamoja wataalamu wa masomo, taasisi za masomo, mashirika ya jamii za umma, kampuni, na wawekezaji kutoka kote ulimwenguni ili kulinda na kukuza haki za uhuru wa kujieleza na faragha katika sekta ya teknolojia ya maelezo na mawasiliano (ICT). GNI inawezesha kazi ya ushirikiano kwa kuweka kiwango cha kiulimwengu cha kufanya maamuzi ya busara, kufanya tathmini huru za jitihada za kampuni, kukuza mazungumzo ya faraghani mionganini mwa wanachama, na kuhudumu kama sauti ya washikadau wengi wanapokumbwa na vikwazo na mahitaji ya serikali. **Tazama orodha kamili ya wanachama na wakaguzi.**



GLOBAL  
NETWORK  
INITIATIVE



## KAMPUNI WANACHAMA WA GNI

- > **KUSHIRIKIANA** na kundi la wahusika tofauti ili kusaidia kuweka kiwango cha kiulimwengu ili kukuza na kulinda haki za uhuru wa kujieleza na faragha.
- > **KUPANUA** na kuimarisha uhusiano na washikadau muhimu wa jamii za umma, kimasomo, na wawekezaji.
- > **KUFIKIA** fursa za kujifunza pamoja na wanachama wengine wa GNI katika mazingira ya umma na kibinagsi, ikijumuisha kuhusu mada nyeti, kwa msingi wa faragha kupitia mradi wetu wa mafunzo ya pamoja.
- > **KUDHIBITI** hatari na kuimarisha ufanyaji maamuzi wa kampuni kupitia utekelezaji wa Kanuni na Miongozo ya Utekelezaji ya GNI.
- > **KUPATA** michango bila kuchelewa katika hatari na fursa za kubadilisha kwa haraka mazingira ya kisheria na kiudhibiti
- > **KUONYESHA** uongozi katika eneo muhimu la sera ya kijamii.



## MAFANIKIO YA GNI

- > **Kutoa mzunguko pekee wa tathmini huru katika sekta ya ICT - imekamilisha mzunguko wake wa tatu mwezi Aprili 2020** - kwa ambao idadi inayoongezeka ya kampuni katika sekta ya ICT imetambua mazoea mazuri, kujadiliana changamoto, na kubadilishana maoni mazuri na wataalamu wa haki za binadamu na kampuni wenza.
- > **Kutoa fursa endelevu kwa ajili ya mafunzo ya pamoja katika mazingira ya faragha**, na kuwezesha kampuni kushiriki katika sera zao za ndani kuhusu jinsi teknolojia mpya zinavyoweza kuathiri uhuru wa kujieleza na faragha. Mwito wa GNI wa mafunzo umejadili mishangao mijpy na inayoendelea ambayo inakumba kampuni za ICT katika mamlaka tofauti kwa ajili ya mahitaji ya serikali ya kuondoa maudhui, kudakiza huduma, maombi ya data za watumiaji.
- > **Kutumia jukwaa lake la kimamlaka ili kushirikiana na watengenezaji sera, washikadau na katika miradi ya kimataifa** kuelekeza mazungumzo kuhusu sera na mazoea ya ICT yanayolinda na kuimarisha haki za binadamu. Hii inajumuisha miradi ya Christchurch Call Advisory Network, Freedom Online Coalition Advisory Network, na Internet & Jurisdiction Policy Network. GNI imefanya ubia na taasisi za aina tofauti, ikijumuisha Council of Europe na pia United Nations Counter-Terrorism Committee Executive Directorate.
- > **Kuwakilisha wanachama wanaoongezeka na wanaoendelea kuwa tofauti**, ikijumuisha kampuni wanachama barani Asia na Ulaya na wasomi, mashirika ya jamii za umma, na wawekezaji kutoka barani Afrika, Ulaya, Amerika Kusini, Amerika Kaskazini, Mashariki ya Kati, na Asia Kusini, ambazo zimeshiriki katika operesheni za kampuni nyanjani.